# FUMO LIYONGO

## Kithaka wa Mberia

Fumo Liyongo anasifika sana katika fasihi simulizi ya Waswahili. Sifa hizo pia zimeingia katika ushairi-andishi ulio na msingi wa ngano za jamii. Katika makala hii nanuia kuongelea sifa za shujaa huyo wa masimulizi na mashairi kama zinavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili na kisha nijaribu kuzifasiri sifa hizo katika muktadha wa mashujaa wa masimulizi kwa jumla.

Miongoni mwa kazi za kishairi ambazo zinazungumzia sifa za Liyongo kwa kirefu ni Takhmisa ya Liyongo na Utenzi wa Liyongo. Katika makala hii kazi ya kwanza itajulikana kama 'Wanji-Wanji' na ya pili kama 'Utenzi.

Katika Wanji-Wanji Liyongo anadhihirika kama jabari na jasiri ambaye hakunywea mbele ya maadui zake hata walipokuwa wengi na wenye silaha kali. Daima alikuwa tayari kukabiliana nao kwa moyo wa ushupavu. Kwani woga ulikuwa kitu cha kuepukana nacho na waoga watu wa kujitenga nao. Msimamo wake ulikuwa kwamba Mungu pekee ndiye aliye na uwezo wa kuangamiza binadamu na wala sio binadamu wengine. Hivyo basi anashauri:

> Wazi ata kicho na wachao sandaye nao
> Nao fawith umuri kwa Mungu anusurao
> Siche ya ziumbe na zituko wakutishao
> Kufa kwa Mungu na shabuka limkutao
> Si kwa walimwengu mivi kikwi ingakufuma

Liyongo hakupigana kwa ajili ya kupenda kupigana au kwa kutaka kusifiwa. Sifa za namna hiyo aliziona ni mbaya. Alipigana kulipokuwa na sababu nzuri ya kufanya hivyo. Inaonekana kwamba miongoni mwa sababu hizi ni utetezi wa cheo. Pia inaelekea kuwa, kwake, kutokuwa na cheo alichokuwa akipigania kulikuwa sawa na kuteremshwa katika ngazi ya hadhi. Alikiona cheo hicho kuwa ni stahiki yake. Tunaambiwa:

*Ana ndimi simba mfiliye jaba na cheo*
*Naipiga kati kawanesa wajibagao*
*Siche aduizo kukutana kwa ungi wao*
*Sichi kikwi chao nami ume ndio nilio moyo*
*Wangu kikwi kwa ajili ya kushagama.*

Haijitokezi wazi iwapo alikuwa anawekewa vikwazo ili asikipate cheo hicho au tayari alikuwa nacho akawa anapokonywa.

Sababu nyingine iliyomshawishi kupigana ni kupinga unyonge na udhalilishaji. Alikuwa si mtu wa kukiri dhila na hakusita kumlipa kwa ubaya aliyemtendea mabaya. Kwa maoni yake, msimamo huo umekubaliwa na Mungu ambaye ameuidhinisha kwa kusema:

Wa ni akabitum fahakibu bi mithiliwa

Tunaweza kutizama sababu hii ya pili kama sura nyingine ya sababu ya kwanza. Hatuelezwi kwa lugha dhahiri mambo aliyoyachukulia kuwa ni madhila na udhalilishaji. Hata hivyo kutokana na habari kwamba alikuwa mkali mno wakati wa kutetea cheo, tunaweza kukisia kwamba, kwa maoni yake, kutokuwa kwake na cheo kilichohusika kulikuwa sawa na kuvunjiwa heshima; jambo ambalo aliliona kama udhalilishaji na utwikwaji wa unyonge. Pengine hivyo ndivyo ulivyomchukiza ulimwengu na kumpa ghadhabu ambazo zilimjaza giza moyoni, kwani tunaambiwa:

*Nionapo ari ulimwengu wanitukiza*
*Moyo ukinayi hata ndani ukawa kiza*
*Na nde mwa kope kozi tule likituuza*
*Simba uwalia kwa kilio akiumiza*
*Kilio kikuu kifishacho mtu huruma.*

Kazi ya pili inayotuelezea sifa za Liyongo ni Utenzi. Kazi hii iliandikwa na Mohamed Kijumwa. Katika Utenzi, ushupavu wa Liyongo katika vita unazidi kutiliwa mkazo. Akiwaelezea Wagala ushupavu huo mfalme wa Pate alimsifia kwa kusema kwamba alikuwa kama simba na kwake kutembea usiku au mchana yalikuwa ni mamoja. Kumtokea mtu ghafla kungesababisha mtu huyo kutapa na

kulia kwa woga. Kukodoa macho yake kungetosha kumfanya binadamu kuzimia. Wagala, ambao pia walikuwa mashujaa wa vita, walicheka kwa dhihaka. Walimwambia mfalme kwamba wangependa kumwona Liyongo. Mfalme alituma akaitwe. Liyongo alikubali mwaliko huo wa kwenda Pate.

Katika maelezo ya ziara hiyo ya Pate picha ya Liyongo tunayoipata ni ile ya mtu mwenye nguvu sana. Kwanza tunafahamishwa kwamba, safari ya kutoka Shaka ambako alikuwa akiishi Liyongo - hadi Pate, ilimchukua siku mbili badala ya siku nne ambazo zingechukuliwa na watu wengine. Pili, alipofika Pate huku amebeba panda tatu, alizipasua mbili kwa pumzi za mapafu yake:

*Liyongo kenda muini*
*akipata mlangoni*
*panda katia kanwani*
*kivuzia kapasua*

*Kiivuzia hakika*
*muini wakashtuka*
*panda ikapasuka*
*Wagala wakasikiya*

*Liyongo asimuhuli*
*akaipiya ya pili*
*pandaye isihimili*
*na ya pili kapasuwa*

Kisa cha tatu katika ziara yake ya Pate ambacho kinaonyesha nguvu nyingi alizokuwa nazo ni kwamba alifika huko akiwa amebeba mkoba uliokuwa na vitu vyenye uzani mkubwa sana. Tunaelezwa:

*Kisa katiti katuwa*
*mkobani akatowa*
*zitu alizotukuwa*
*nyumba ndima nisikiya*

*Katowa kinu na m'ti*
*na jiwe la kupanza kuti*
*na zunguze si katiti*
*na mawe ya kupikiya*

MAKTABA
TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

*Na kipeto cha mtama*
*na ya nazi makoroma*
*Wagalla wakaatama*
*ajabu ikawangiya*

Picha ya uwezo mkubwa wa kimwili wa Liyongo inaimarishwa hata zaidi tunapoonyeshwa kimo chake akilinganishwa na Wagala. Ingawaje:

*Wagalla hao yuwani*
*ni wakuu wa mwituni*
*kabila ya Sulutwani*
*mashujaa wote pia*

umbo lao lilikuwa dogo sana lilipolinganishwa na lile la Liyongo kwani:

Zimo zao hukoma ondo.

Tunasimuliwa kishairi kwamba mfalme hakumpenda Liyongo, kwani alihofu kwamba angempokonya ufalme. Mfalme aliamua kumuua ili kuepukana na uwezekano huo. Liyongo aligundua nia hiyo ya mfalme. Kwa hivyo, alitoroka na kuingia bara. Mfalme aliwaagiza Wasanye na Wadahalo kumfuata huko na kumuua kwa malipo. Kwa sababu ya ushupavu wake katika vita, Wasanye na Wadahalo walijua kwamba haingewezekana kumuua kwa njia ya ana kwa ana. Kwa hivyo, walifanya njama ya kumuua kwa hila. Walipoenda bara walimwendea kwa 'urafiki' wakamwomba awe pamoja nao. Walipanga wawe wakila makoma, hivi kwamba, kwa zamu, kila mmoja wao (akiwemo Liyongo) angepanda juu ya mkoma na kuyatunda makoma. Kila mmoja miongoni mwao isipokuwa Liyongo alitekeleza tarajio la mpango huo. Ikabakia zamu ya Liyongo. Siri yao ilikuwa kwamba, Liyongo apandapo mkoma, wamfume mishale kwa pamoja. Hali ya kuwa juu ya mkoma ingemzuia kupigana.

Kwa bahati nzuri Liyongo alikuwa sio tu mkakamavu wa mwili bali pia mkakamavu wa akili. Alitambua nia yao. Aliitambua nia hiyo kwa kuwa mkoma waliomchagulia kupanda ulikuwa mrefu sana. Badala ya kuupanda ule mkoma, tunaelezwa:

*Akawaambia ngojani*
*akatowa mkobani*
*chembe katia ngweni*
*makoma kiwanguliya*

*Achangusha ngaa ndima*
*ni mangi mno makoma*
*kwa wut'e wakaatama*
*ajabu zikawangiya*

Hivyo basi, njama yao haikufaulu.

Licha ya Liyongo kuwa na ujasiri wa moyo, nguvu za mwili na wepesi wa akili, pia alikuwa stadi katika gungu na mwao. Mfalme alijua ukweli huo. Alionelea kwamba maandalizi ya mwao ambapo Liyongo angealikwa ungekuwa mtego mzuri wa kumshika. Basi uliandaliwa mwao na kualikwa Liyongo ambaye wakati huo alikuwa tayari amerejea mjini baada ya kudanganywa kwamba hakukuwa na hatari tena. Alipohudhuria ngoma hiyo, watu wa mfalme walimwendea kwa silaha, wakamshika na kumuweka gerezani.

Ingawaje baadhi ya watu walishauri asiuliwe kwani kwao alikuwa kama ngao dhidi ya maadui zao, mfalme alikuwa akimwogopa sana hivi kwamba alionelea kwamba kumuua ndilo lililokuwa jambo la busara. Siku tatu kabla ya kutimizwa kusudio la kuuliwa Liyongo, mtumishi wa mfalme alitumwa kumuuliza jambo ambalo angependa kabla ya kuuliwa. Liyongo aliomba kuandaliwa mwao na gungu. Mfalme alikubali ombi lake na kwa hivyo mwao na gungu zikaandaliwa.

Kwa mara nyingine tena akili arifu ya Liyongo ilimuwezesha kuepukana na kifo. Kwa ushairi alimtuma mtumishi ambaye alikuwa akimletea chakula gerezani kwamba akamwambie mama yake (Liyongo) aupike mkate wa wishwa na humo ndani afiche tupa ampelekee ili aitumie kukerezea minyororo aliyokuwa amefungwa kwayo gerezani. Kwa mujibu wa J. Knappert (1979), sababu ya kutaka mkate upikwe kwa wishwa ni kwamba kila mama yake alipomtuma mtumishi Sada kumpelekea mwanawe chakula

kizuri askari washika doria walimpokonya Sada chakula hicho na kukila. Sada alipouleta mkate wa wishwa (ukiwa na tupa ndani yake) askari walitukana kwa dhihaka na kumruhusu Sada kumpelekea Liyongo. Yaliyofuata baada ya hapo ni haya:

*Hata usiku kufika*
*matezo wakayandika*
*kama ada wakaweka*
*t'asa, pembe, siwa piya*

*Na ngoma na nyingi kusi*
*kusisalie unasi*
*ikawa kama ħarusi*
*watu wakiangaliya*

*Wut'e wakakutanika*
*mahala pakatandikwa*
*na uzuri wakaweka*
*deuli na subahiya*

*Kulla nyimbo zizidipo*
*na ngoma zitakatapo*
*alikizitinda hapo*
*pingu na minyoo piya*

*Zilipo kikaza kusi*
*alikikata upesi*
*hata zikikoma basi*
*inukani kawambiya*

*Wakiinuka kuteza*
*Liyongo akatokeza*
*Khaufu zaliwakaza*
*mbiyo zikawapoteya*

*Kwa wut'e wakakimbiya*
*ħapana alosaliya*
*Liyongo kaitokeya*
*mabarani kareja*

Baada ya majaribio haya mawili ya kumuua Liyongo

kutofua dafu, mfalme alibadili mbinu zake. Aliamua kumuua kwa kutumia mwanawe (Liyongo). Huku akiahidiwa kuozwa bintiye mfalme kama kiinua-mgongo, mwanawe Liyongo aliombwa na mfalme amuue babake. Hatua ya kwanza ya mwanawe Liyongo katika harakati za kutekeleza ombi la mfalme, ilikuwa kuchunguza kilichoweza kumuua babake. Kwa mujibu wa masimulizi, ni kitu kimoja tu ulimwenguni ambacho kingeweza kumuua Liyongo, nacho kilikuwa kudungwa sindano ya shaba kitovuni. Habari hiyo muhimu mwanawe Liyongo aliipata kutoka kwa babake mwenyewe. Habari hiyo ilipofikishwa kwa mfalme aliifurahia sana na kuagiza sindano ya shaba ifuliwe mara moja. Mfalme alimfadhili mwanawe Liyongo kwa takrima nzuri sana, jambo ambalo lilimzidishia mwanawe Liyongo tamaa na matumaini ya kuozwa binti ya mfalme. Tunafahamishwa kwamba:

*Siku kumi akaketi*
*kipowa nzuri kuti*
*kusingie tafauti*
*ila mambo kuongeya*

*Kijana kafurahika*
*tamaa zikamshika*
*na kuowa ni hakika*
*hawa watanitendeya*

*Akaweka na uposi*
*kama ni bwana harusi*
*kulla siku kianishi*
*kipumbaza mno ghaya*

Baada ya siku kumi, mwanawe Liyongo alikabidhiwa sindano ya shaba, akasafiri hadi kwa babake, na alipopata fursa mwafaka, alimdunga sindano hiyo kitovuni na kutoroka. Tunaelezwa kwamba Liyongo alichukua zana zake za vita hadi kisimani ambako alijifia huku mshale kauweka kwenye upinde.

Kama hatua ya kwanza katika harakati za kufasiri visa na sifa za Liyongo, ningependa kutaja kwamba sifa za namna hiyo au hata kubwa zaidi hupatikana katika ngano za jamii nyingine. Hivyo basi, hatupaswi

kuyatizama maelezo juu ya Liyongo kama ni mambo ya kipekee ulimwenguni. Kama tutakavyoona huko mbele katika makala hii, sifa kama hizo katika masimulizi ya kijamii, ni jambo la kutarajiwa katika muktadha fulani wa kihistoria.

Kabla ya kufafanua muktadha wa kihistoria ninaoongelea, ningependa kuzungumzia ngano nyingine katika jamii tofauti ambayo ina vituko vikubwa kama vile vya ngano ya Liyongo. Mfano mzuri wa ngano kama hiyo ni ile ya Sundiata. Ngano hiyo inahusu mhusika anayejulikana kama Sundiata na ambaye ni shujaa wa jamii ya kale ya Mali. Ngano hiyo imechapishwa katika kitabu kiitwacho *Sundiata: An Epic of Old Mali* cha D.T. Niane. Katika kitabu hicho tunafahamishwa nguvu nyingi alizokuwa nazo Sundiata (au Mari Djata).

Nguvu hizo zinadhihirika vizuri zaidi katika sura inayoelezea jinsi Mari Djata alivyoanza kutembea. Alichelewa kuanza kutembea. Hata baada ya kufikia umri wa miaka saba aliendelea kutambaa kwa kutumia magoti na mikono. Jambo hili lilimhuzunisha sana mamake Sogolon Kedjou. Huzuni hiyo ilifikia kilele chake siku ambapo Sogolon alimwendea Sassouma Berete, mke mwenza, ili amsaidie majani ya kupika. Sassouma alimkubalia Sogolon kuchukua majani bali kwa namna ambayo ilimkasirisha sana Sogolon. Kwa dhihaka, Sassouma alimkumbusha kwamba mwanawe (yaani Mari Djata) hakuwa na uwezo wa kutembea katika umri wa miaka saba, tofauti na mwanawe ambaye aliweza kutembea akiwa na umri huo na ambaye ndiye aliyekuwa amechuma majani aliyokuwa akikubaliwa kuchukua. Sogolon hakuweza kustahimili matusi hayo. Aliondoka kwa Sassouma na kurejea kwake akiwa na uchungu mwingi moyoni. Alimkuta Mari Djata ameketi nje ya nyumba anajilia chakula. Huku akilia, Sogolon alichukua ukuni na kumpiga Mari Djata. Mari Djata aliushika ukuni huo na kumuuliza mamake kilichokuwa kikimliza. Sogolon alimweleza mwanawe kilichotendeka, ambapo Mari Djata alimwahidi kwamba angetembea siku hiyo hiyo. Aliagizia wafuaji chuma wa marehemu babake wafue mtalimbo wa chuma kadiri iwezekanavyo. Mtalimbo kama huo tayari ulikuwemo katika

banda la ufuaji. Mfuaji mkuu, Farkourou, aliwaita wanafunzi wake sita na kuwataka waupeleke mtalimbo huo kwa Sogolon. Wanafunzi walitekeleza agizo hilo.

Mari Djata alipomaliza kula, mambo makubwa sana yalizuka. Tunasimuliwa kwamba:

> *Wanafunzi wa ufuaji walikuwa bado wapo, Sogolon alikuwa ametoka nje na kila mtu alikuwa anamtizama Mari Djata. Alitambaa kwa miguu na mikono na kuufikia mtalimbo wa chuma. Huku akijihimili kwa magoti na mkono mmoja aliuchukua mtalimbo kwa mkono wa pili bila taabu yo yote na kuusimamisha. Wakati huu alikuwa amejihimili kwa magoti yake na kuushikilia mtalimbo kwa mikono yake yote. Kimya kikubwa kilikuwa kimewakumba wote waliokuwepo. Mari Djata aliyafumba macho yake, akashika vilivyo, misuli yake ikajikaza. Kwa mshtuo mkali aliusukumia uzani wake kwenye mtalimbo na magoti yake yakainuka kutoka chini. Sogolon alimkazia macho na aliitizama miguu ya mwanawe ambayo ilikuwa ikitetemeka kama kwa pigo la umeme. ...jasho lilikuwa likimtiririka kutoka katika panda la uso. Kwa mkakamko mkubwa alijinyosha na kusimama kwa miguu yake - lakini ule mtalimbo mkubwa ulipinda na kuchukua umbo la uta! ... Baada ya kupumua, mwanawe Sogolon aliuangusha mtalimbo ... Hatua zake za mwanzo zilikuwa zile za shujaa.*

Hivyo ndivyo alivyoanza kutembea Sundiata. Baada ya hapo aliuendea mbuyu mchanga uliokuwa nyuma ya Niani na ambapo ndipo watoto wa mjini walipokuwa wakienda kuwachumia mama zao majani. Kwa nguvu zake zote Sundiata aliung'oa mbuyu huo, akajitwika mabegani, na kurejea kwa mamake ambapo aliutupa mbele ya nyumba na

kusema:

> *Mama haya hapa majani ya mbuyu*
> *kwa manufaa yako. Kutoka leo*
> *itakuwa ni nje ya nyumba yako ambapo*
> *wanawake wa Niani watakuwa*
> *wakija kuchuma majani.*

Ingawaje Mandingo ambao husimulia ngano ya Sundiata na Waswahili ambao husimulia ngano ya Liyongo wanaishi katika jamii mbili tofauti tunaona kwamba kuna jambo ambalo linazifanya ngano hizo mbili kufanana. Jambo hilo ni ile hali ya kuwa ngano zote mbili zinazimulia kuhusu nguvu za kimwili zilizo nje ya uwezo wa binadamu halisi: Liyongo alipasua panda kwa pumzi za mapafu! Alibeba mkoba uliokuwa na vitu vilivyojaza nyumba nzima! Naye Sundiata, katika umri wake mdogo, alikuwa na nguvu zilizosababisha kupinda mtalimbo wa chuma ambao uliwachukua watu sita kuubeba! Kama wahakiki wa ngano za mashujaa tunapaswa kudadisi kinachosababisha hali hiyo ya uwezo wa juu sana miongoni mwa mashujaa wa masimulizi. Je, uwezo huo ni ukweli halisi au ni ubunifu?

Kwa jumla katika ngano za mashujaa, sifa za shujaa hutiliwa chumvi na umma unaojitambulisha naye na ambao unaonea fahari kubwa vitendo vyake, hususa vile vya kishujaa. Hali hiyo ya kutia chumvi visa mahususi vya kihistoria na sifa maalum za mhusika wa kihistoria huzaa na kukuza shujaa mwingine mwenye sifa sambamba na shujaa wa kwanza bali zilizokwezwa mara kadha wa kadha katika ngazi ya sifa. Hivyo basi, msomaji wa *Wanji-Wanji* na *Utenzi* apaswa kutambua kwamba katika Liyongo kuna Liyongo wawili: Mmoja ni Liyongo wa kihistoria ambaye aliwahi kuishi katika sehemu za kaskazini ya mwambao wa Kenya. Liyongo wa pili ni yule wa ngano na ushairi ambaye ametokana na chuku ya masimulizi. Baina ya hao Liyongo wawili; yule wa kifasihi ana uwezo mwingi kuliko yule wa kihistoria; vile vile ana uwezo mkubwa kuliko binadamu halisi kwani si binadamu halisi. Kwa hivyo, kwake si hoja kupasua panda kwa pumzi za mapafu wala kubeba mkoba uliokuwa na kinu, mchi, jiwe

la kupanza kuti, vyungu kadha wa kadha, mawe ya kupikia, kipeto cha mtama na madafu ya nazi! Huyo ndiye Liyongo ambaye hangeulika kwa kitu kingine cho chote ila kudungwa sindano ya shaba kitovuni.

Shujaa wa kihistoria huzaa shujaa wa kifasihi pale kunapokuwa na mkinzano baina ya makundi ya jamii moja au baina ya jamii tofauti. Mkinzano huo unaweza kuwa umesababishwa na tofauti za kiitikadi kijamii, kisiasa, kiuchumi, na kadhalika. Mikinzano ya namna hiyo ndiyo imesababishwa kuzuka kwa mashujaa wa matawi mbali mbali ulimwenguni wakiwepo Liyongo, Sundiata, Mwindo, Shaka, Muhamadi na pia yule shujaa maarufu wa kiyahudi ajulikanaye kama Yesu Kristo.

Imedaiwa kwamba Liyongo wa kihistoria alikuwa bingwa wa ushairi na stadi wa *gungu* na *mwao*. Katika J. Knappert (1979) kumekusanywa mashairi ambayo Liyongo anadaiwa alitunga. Miongoni mwa mashairi hayo ni Wanji-Wanji.

Wanji-Wanji ni shairi la bahari ya takhmisa. Inasemekana kwamba tungo za takhmisa, hasa katika hali yake asilia katika ushairi wa Kiarabu, hutungwa na washairi wawili. Mshairi wa kwanza hutunga mistari miwili ya mwisho katika kila ubeti naye mshairi wa pili hujaliza mistari mitatu ya mwanzo bila kupotosha maana au kutatiza muwala. Kwa mujibu wa J. Krappert (1979), Liyongo ndiye aliyetunga mistari miwili ya mwisho kati beti za Wanji-Wanji. Hata hivyo, J. Knappert anadai kwamba Liyongo hakuchangia utunzi wa beti mbili za mwisho katika utungo huo wa beti ishirini na nane. Kuna wengine wanaodai kwamba Wanji-Wanji ilitungwa na mtunzi wa Inkishafi, yaani Sayyid Abdalla Ali Nasir. Miongoni mwa wenye kauli hiyo ni W. Hichens (1972), A. Abdalla, na E. Kezilahabi (1983). Nadhani miongoni mwa sababu zinazowafanya baadhi ya watu kufikiria kwamba Wanji-Wanji ilitungwa na Sayyid Abdalla Ali Nasir ni beti mbili za mwisho katika utungo huo zisemazo:

*Na mwenye kutunga mbaarifu yakwe ismu*

*Ni Abdalla muyuweni mumfahamu*
*Ibun Ali bun Nasiri mwenye makamu*
*Fari ya Makka shimukati lao Farimu*
*Fungu la Muthari, Mutalibu na Hashima*

*Nipulikizani nasabuye niwakhubiri*
*Ni Ali Shekhi maulana Abubakari*
*Ibun Salima Maunsabuya kukhitari*
*Mungi wa karama barubani na mashuhuri*
*Kwa zamani zakwe hakwalina kamaye kama*

Suala la aliyetunga au waliotunga Wanji-Wanji lina utata ambao si rahisi kuupa suluhu. Kwa jumla kuna uwezekano kadha wa kadha kuhusu utunzi wa utungo huo. Uwezekano wa kwanza ni kuwa Wanji-Wanji ilitungwa na mtunzi mmoja. Tungelikuwa na hakika kwamba hiyo ndiyo hali ya mambo tatizo letu juu ya utunzi wa utungo huo lingelikuwa si kubwa kama lilivyo hivi sasa. Swali ambalo tungelijishughulisha nalo lingelikuwa iwapo Wanji-Wanji ilitungwa na Liyongo, Sayyid Abdalla au mtunzi mwingine wa tatu. Kwa bahati mbaya, kuna mambo mbali mbali katika utungo huo ambayo yanatuelekeza kufikiria kwamba pengine Wanji-Wanji ilitungwa na zaidi ya mtunzi mmoja na pengine katika nyakati tofauti. Tutizame ubeti wa kwanza:

*Nabudi kawafi takhmisa kidiriji*
*Niwathihishe izagale kama siraji*
*Ili kufuasa ya Liyongo simba wa miji*
*Ai wanji wanji nazawanji kisiza wanji*
*Na kadiliza kasiliza, mwanangwa mwema*

Ninapousoma ubeti huu, akili yangu hufuata vyema maana inayotiririka katika mishororo mitatu ya mwanzo, lakini iingiapo kwenye mishororo miwili ya mwisho inagubikwa ghafla na gubigubi zito la ukungu. Hali hiyo inaposadifu, ninajikuta katika hali ya kuuliza maswali: Je ubeti huo ulitungwa na mtunzi mmoja au watunzi wawili hivi kwamba mmoja alitunga mishororo miwili ya mwisho naye wa pili akatunga mishororo mitatu ya mwanzo? Ni kwa nini mafungu hayo mawili ya mishororo yanatofautiana kwa upande wa ugumu wa lugha? Je,

mishororo yote mitano ilitungwa wakati mmoja au nyakati tofauti? Inawezekana mishororo miwili ya mwisho ikawa ni ya zamani zaidi kuliko mishororo mitatu ya mwanzo? Inawezekana kuwa hiyo ndiyo sababu inayoipa mishororo miwili ya mwisho ugumu zaidi ikilinganishwa na mishororo mitatu ya mwanzo? Kwa hivi sasa tuyaweke kando maswali hayo. Kwanza tutizame kwingineko.

Katika ubeti huo wa mwanzo, hususa mishororo mitatu ya kwanza, inaonekana kama kwamba anayezungumza si yule mwenye sifa zitakazoelezewa katika utungo bali mtu mwingine ambaye anafahamu kuwepo kwa sifa hizo. Anayezungumza anadiriji takhmisa ya *ukawafi* 'Ili kufuasa ya Liyongo simba wa miji.'Sauti hiyo inatujia tena katika ubeti wa tatu kutoka mwisho ambapo tunaambiwa:

*Tamati nishiza takhmisi kinaathimu Ya Liyongo Fumo nimaziye kuikhirimu....*

Baina ya kingo hizo mbili ambazo tunaweza kuziita utangulizi na hitimisho, tunapewa sifa mbali mbali za Liyongo. Sifa hizo zinatufikia kwa sauti ya nafsi ya kwanza, umoja. Kwa mfano, tunaelezwa:

*Naitenda mja kwa wenzangu kupata sono*
*Wala sina yambo siwatayi kwa mavongono*
*Bali sikubali lenye thila na matukano*
*Ni mwofu watanishikapo naaa mno*
*Ni mui wa kondo sikiapo mbi kalima*

Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba tuna sauti mbili katika Wanji-Wanji, sauti ya kwanza ikiwa ni ile inayotoa utangulizi na hitimisho, nayo ya pili ile inayofafanua sifa mbali mbali za Liyongo. Katika sauti ya utangulizi na hitimisho Liyongo ni 'yeye' ilhali katika sauti inayofafanua sifa zake, Liyongo ni 'mimi'. Kwa mfano:

*Naapa kwa Anjili na Zaburi ile kiapo*
*Simekengeufu pindi shari liwagazapo*
*Naye keeza moyo katokoza shari lilipo*

*Mtetea cheo mwenye cheo ateteapo*
*Hambiwi ni mwi hatta roho nengakoma.*

Tunapotilia maanani suala hili la sauti mbili katika utungo akili zetu zinaelekezwa kwenye mizungu mbali mbali. Kwanza, ama Wanji-Wanji ilitungwa na watunzi wawili, mmoja akiwa Liyongo mwenyewe na wa pili akawa ni yule aliyeandika utangulizi na hitimisho; au pili, Wanji-Wanji ilitungwa na watu wawili, mmoja akiwa amejiweka katika hali ya Liyongo na kuiazima sauti yake na wa pili akiwa ni yule aliyetoa utangulizi na hitimisho; au tatu, Wanji-Wanji ilitungwa na mshairi mmoja ambaye hakuwa Liyongo lakini ambaye aliichukua sauti ya Liyongo baada ya utangulizi na kuitupa tena kabla ya hitimisho.

Turejee tena suala la tofauti za ugumu wa lugha iliyotumiwa katika utungo. Lugha iliyotumiwa katikati ya inaonekana nyepesi kuliko ile ya:

*Ai wanji wanji nazawanji kisiza wanji*
*Na kadiliza kasiliza, mwanangwa mema*

bali ngumu kuliko lugha iliyotumiwa katika mishororo mitatu ya mwanzo katika ubeti wa kwanza ana vile vile ile iliyotumiwa katika beti tatu za mwisho. Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba Wanji-Wanji ina viwango vitatu vya ugumu wa lugha; hali inayofufua tena maswali yangu ya huko nyuma. Ningependa kujaribu kuyajibu maswali hayo kwa kauli ya kijumla: Inaonekana kama kwamba Wanji-Wanji ilitungwa na zaidi ya mtunzi mmoja katika nyakati mbali mbali hivi kwamba kazi tuliyo nayo sasa ina majalizo ya hapa na pale. Kwamba beti mbili za mwisho katika utungo huo zinadai kwamba mtunzi wa utungo huo ni Sayyid Abdalla ni jambo ambalo, kwa maoni yangu, halipaswi kuchukuliwa kama ithibati ya hoja kwamba Wanji-Wanji ilitungwa naye. Kuna uwezekano kwamba beti hizo ziliongezwa katika utungo na mtu mwingine ambaye aliamini kwamba utungo huo ni kazi ya Sayyid Abdalla. Pia kwamba sifa za Liyongo katikati ya utungo huo zinaelezewa kwa nafsi ya kwanza, umoja, yaani katika hali ya 'mimi', ni jambo ambalo halitoshi

kutufanya kuchukulia kwamba usemi huo ni wa Liyongo mwenyewe. Katika fasihi si muhali kwa mwandishi kujitia katika hali ya mtu mwingine na kuzungumza 'akiwa mtu huyo.'

Sababu ya kujitosa katika uzungumzi huu wa mzunguko juu ya utunzi wa Wanji-Wanji ilikuwa kuchunguza iwapo shairi hilo lilitungwa na Liyongo, jambo ambalo lingethibitisha madai kwamba Liyongo (wa kihistoria) alikuwa mshairi. Sioni jambo lo lote katika utungo huo ambalo linatuonyesha pasipo na shaka kwamba ulitungwa na Liyongo. Hivyo basi, hatuwezi kutumia utungo huo kuufikia uamuzi kwamba Liyongo alikuwa mshairi.

Nilitaja huko nyuma kwamba licha ya Liyongo kudaiwa alitunga Wanji-Wanji, pia hudaiwa kwamba alitunga mashairi mengine. Kama nilivyodokeza, baadhi ya mashairi hayo yamekusanywa na J. Knappert (1979). Baadhi ya mashairi hayo yana lugha ambayo tunaweza kusema inalingana na kiwango cha pili miongoni mwa viwango vitatu vya lugha ya Wanji-Wanji. Mfano mzuri ni fungu lifuatalo lenye mishororo minne:

*Noa kifua na nguoza mbwenepo mai*
*Kateka kinywa nikisaza, nyota sisii*
*Aniombao sikuiza, nduza ahii*
*Sina la kambi, namba nywai, sikuyasiza.*

Mashairi mengine yana lugha nyepesi (na kwa maoni yangu ya majuzi zaidi) kuliko fungu la hapo juu. Mifano mizuri ni beti tatu zifuatazo, kutoka mashairi matatu tofauti:

*We mteshi ulo mnazini*
*Nipe uchi ulio uchungu*
*Nitekea kwa kikasikini*
*Teshewèo na mgema wangu...*
*Ai mwezi kuwawato*
*Kuwania makutani*
*Kuwawia shaha Shanga Shaha Ozi yu gizani*
*Chui hoho! chui Manga...*
*Ewe mwana nyamaa utue*

*Nikutuze nguo za Hijazi....*

Sioni sababu ya kunifanya niseme kwa hakika kwamba mashairi yanayowakilishwa na beti hizo tatu yalitungwa na mtunzi aliyetunga shairi linalowakilishwa na ubeti wa kwanza. Pia sioni thibitisho la kunifanya nidai kwamba shairi hilo lilitungwa wakati mmoja na mashairi hayo mengine.

Pengine Liyongo alikuwa mshairi. Pengine alitunga baadhi ya sehemu za Wanji-Wanji na vile vile mashairi mengine. Hata hivyo, kwa maoni yangu, hatuna ithibati ya kutuvusha ng'ambo nyingine ya ukingo wa 'pengine.' Kama nilivyojaribu kuonyesha hapo juu, hatuna ithibati kama hiyo ama katika Wanji-Wanji au katika mashairi yaliyomo katika J. Knappert (1979).

Utafiti juu ya nyakati maalum alipoishi Liyongo na mkinzano au mikinzano mahususi ambamo alishiriki ni miongoni mwa masuala muhimu sana katika fasihi simulizi ya Waswahili na Wapokomo na vile vile historia ya mwambao wa pwani ya Kenya, hasa, mwambao wa kaskazini. Kufikia hivi leo, habari za kihistoria tulizo nazo kuhusu Liyongo ni za makisio tu. Kwa mfano inakisiwa aliishi miaka ya karne ya kumi na tano au kumi na sita. Pia kuna kubahatisha kwingi juu ya mkinzano ambamo Liyongo alishiriki kama mmojawapo wa wahusika wakuu. Kwa jumla inaonekana kwamba mkinzano huo ulihusu uongozi. Mpaka sasa haijawa wazi iwapo mzozo wenyewe ulikuwa baina yake na kaka yake Daudi Mringwari au baina yake na mfalme wa Pate. Hata hivyo, vyo vyote iwavyo, inaonekana vizuri kuchukulia, kama baadhi ya watu wanavyofanya, kwamba Pate ilishiriki katika mzozo huo kwa namna moja au nyingine. Habari zilizomo katika Utenzi zinatuelekeza kwenye uamuzi kama huo.

**TANBIHI**

1. Nimeupa utungo huu anwani ya "Wanji-Wanji" kutokana na mshororo wa nne katika ubeti wa kwanza.

2. Dondoo zote za Wanji-Wanji zilizomo katika makala hii zimetolewa kwenye nakili ya utungo huo iliyopigwa taipu na kutoleshwa nakala na mtambo wa 'cyclostyling.'

3. Tafsiri yangu inatokana na tafsiri ya Kiingereza ya G.D. Pickett, Tafsiri hiyo ya G.D. Pickett imetokana na tafsiri ya Kifaransa ya D.T. Niane iliyotokana na masimulizi katika lugha ya Mandingo.

4. Kama 3 hapo juu.

5. Katika makala ya S.A. Kandoro (1983) tunaambiwa: Na kulingana na kanuni za ushairi wa Kiarabu ni kuwa takhmisa hutungwa na watu wawili. Vilivyo ni kwamba mshairi wa kwanza huitunga mistari *miwili ya mwisho* ya ubeti na mshairi wa pili huitunga mistari *mitatu ya mwanzo,* ya ubeti, na kwa kutumia kina cha mstari wa kwanza (uliotungwa na yule mshairi kwanza) bila kupoteza maana iliyokusudiwa na huyo mshairi wa kwanza na bila kuvuruga mtiririko wa habari. Ubeti huo hutungwa kwa namna ambayo lau utaiondoa ile mistari mitatu ya mwanzo iliyoongezwa na mshairi wa pili, ile mistari miwili ya mwisho iliyotungwa na mshairi wa kwanza, hubakia na maana yake kamili... Utungo huu ulipoingia katika ushairi wa Kiswahili kanuni iliyobakia (na ambayo mpaka leo yafuatwa) ni hiyo ya kwanza tu - ya ubeti kuwa na mistari mitano.

Maoni hayo yametolewa na S.A. Kandoro katika sehemu ya makala yake inayoongelea utafiti wa A. Abdalla juu ya ushairi na yametolewa kwa namna ambayo ni vigumu kujua ikiwa ni ya S.A. Kandoro mwenyewe au ni ya A. Abdalla.

6. Maoni ya A. Abdalla kuhusu suala hili yamenukuliwa na S.A. Kandoro (1983).

7. J. Knappert (1979) anasema:

Pengine ni vyema kuichukulia tarehe ya kifo cha Liyongo kama 1690 au mapema kuliko hivyo.... Profesa Freeman Grenvile anamuweka Liyongo katika mwaka wa 1580 hivi. Pia James Kirkman anaamini pengine aliishi 1600 hivi. (Tafsiri yangu).

Naye J.V. Allen (1984) anasema:

Basi Liyongo wa kihistoria alikuwa mfalme wa mwisho wa Ozi aliyepinduliwa na majeshi yaliyoongozwa na Pate katika miaka ya mwisho wa karne ya kumi na sita.

8. Tizama J. Knappert (1979: 67) na J.V. Allen (1984).

9. Tizama J. Knappert (1979), J.V. Allen (1984) na E. Kezilahabi (1983).

**MAREJEO**

1. Allen J.V. 1984 "Fumo Liyongo: Swahili Poet - King in History and Folklore" Makala iliyotolewa katika kongamano la Historical Association of Kenya.

2. Kandoro S.A. 1983 Hatua Mbali Mbali za Kubuni na Kutunga Shairi la Kiswahili" Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi*. Dar es Salaam: Taasisi ya

Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

3. Kezilahabi E. 1983 "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

4. Kijumwa M. 1913 "Utenzi wa Liyongo"

5. Knappert J. 1979 *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology* Nairobi: Heinemann Educational Books.

6. Niane D.T. 1965 *Sundiata: An Epic of Old Mali* London: Longman Group Limited.

7. - Wanji-Wanji"

## MAONI JUU YA MAKALA KUHUSU "FUMO LIYONGO"

**M.M. Mulokozi**

Nimesoma makala hayo kwa makini, na nina maoni yafuatayo:

1.1 Mwandishi anakusudia kujadili sifa za Liyongo kama shujaa wa masimulizi, na kuonyesha kwamba sifa hizo ni za kiulimwengu na hupatikana katika masimulizi ya mataifa mengine.

1.2 Mwandishi anabainisha sifa 5 alizo nazo Liyongo:

(a) Nguvu za kimwili
(b) Ujasiri/Ushupavu
(c) Nasaba (bora)/cheo
(d) Akili/Ujanja
(e) Usanii (ni bingwa wa ngoma na ushairi)

1.3 Mwandishi anatumia utungo wa "Wanji-Wanji" na "Utenzi wa Fumo Liyongo" kuthibitisha kuwa Liyongo anazo sifa hizo. Kadhalika, anatumia utenzi wa *Sundiata* kuonyesha kuwa shujaa wa utenzi huo vilevile anazo sifa hizo.

1.4 Mwisho, mwandishi anajaribu kuchunguza sababu za shujaa wa masimulizi kupewa sifa hizo, na sababu za kutoka kwa mashujaa wa tendi. Anasema mashujaa hao hutokana na mikinzano ya kijamii.

1.5 Mwandishi anagusia pia mjadala kuhusu tarehe ya Liyongo (wa historia) na kujadili dai kuwa alikuwa mshairi. Anatuambia ushahidi tulio nao hadi wakati huu hauthibitishi kama Liyongo aliishi katika karne ya 15-16 kama wanavyodai baadhi ya wataalamu, na hauthibitishi kuwa alikuwa mshairi.

2. Maoni

2.1 Mwandishi anaona sifa 5 tu za mashujaa wa tendi. Zipo nyingine ambazo hazioni, k.m. ukali, ukatili, kupenda haki, hekima, uwezo wa kiume (urijali) n.k. Baadhi ya mashujaa vilevile huwa na sifa za "uungu-mtu", k.m. Yesu, Gilgamesh, Achilles), ushujaa wa kiroho/kisufii, n.k. Hivyo, mashujaa wa tendi duniani si wa aina moja. Ipo haja ya kuonyesha Liyongo anaingia katika kundi lipi. Mfano wa Sundiata hautoshi kuthibitisha kuwa Liyongo ana sifa za kiulimwengu/kijumla; inatakiwa mifano mingi zaidi kutoka mataifa mengine.

2.2 Si kweli kwamba "Sundiata" ni ngano. Sundiata ni utendi simulizi. Masimulizi ya Niane (1965) ni muhtasari tu wa utendi huo ambao uliimbwa na mayeli *(griots)* wa Mali.

2.3 Nakubaliana na kauli ya mwandishi kuwa shujaa wa historia katika tendi hugeuzwa kuwa shujaa wa fasihi kwa kuyatia chumvi maisha na matendo yake (uk. 12). Kwa *kiasi fulani* ni kweli pia kuwa mikinzano ya makundi ya kijamii huweza kuzua mashujaa wa fasihi. Hata hivyo, nadhani tunahitaji kuwa waangalifu zaidi tunapojadili mashujaa wa tendi katika muktadha wa kijamii. Si kila shujaa anatokana na mikinzano ya kijamii. Kwa mfano, hapa Afrika tunao mashujaa wanaotokea kwa sababu ya mkinzano wa asili kati ya jamii na maumbile asilia. Mashujaa wa aina hiyo huwakilisha jamii nzima iliyoungana kwa lengo moja la kupambana na adui ambaye si binadamu (k.m. Masalakulangwa: Wasukuma; Ssesota: Waganda; Hiawatha dhidi ya Dubu: Wahindi wa Marekani, n.k.)

2.4 Nadharia ya mwandishi katika 2.3 hapo juu inatuelekeza katika nadharia ya kina Chadwick, Bowra na wenzao ya "Heroic Age" (zama za ushujaa) ambayo siku hizi wataalamu wengi wa masimulizi wanaikataa. Sidhani kuwa mikinzano ya kijamii husababishwa na tofauti za kiitikadi (uk. 13). Huenda kinyume chake ndiyo sahihi.

2.5 Masuala yahusuyo sifa za kishairi za Fumo Liyongo yamejadiliwa vizuri. Nakubaliana na mwandishi kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kuwa Liyongo alitunga "Wanji-Wanji" na mashairi mengine yanayodaiwa kuwa ni yake. Jambo ambalo lingesisitizwa hapa ni kwamba Liyongo ni "shujaa wa kitamaduni" (culture hero); hivyo yeye ni kiini cha masimulizi, nyimbo, majigambo, ngoma, n.k. ambayo hufanywa na Waswahili na watu wengine kwa kuyahusisha na jina lake. Si lazima yeye mwenyewe awe ametunga mambo hayo.
-Kuhusu "Wanji-Wanji" (Takhmisa ya Liyongo), kuna uwezekano, kama asemavyo mwandishi, kuwa utenzi huo ulitungwa ama na watu wawili ama na Sayyid Abdalla bin Nasir pekee, n.k. Ili kupata uhakika zaidi juu ya hilo, ingefaa mwandishi atumie mbinu za taaluma ya mitindo (stylistics) na fomula-simulizi (oral formula). Mbinu hizo zikitumiwa vizuri huweza kudhihirisha kama mtunzi ni mtu yule yule au ni watu mbalimbali. Kwa kuwa tunayo mashairi mengine ya Sayyid Nasir (k.m. Inkishafi), jambo hilo lisingekuwa gumu. Masuala kama ya mabadiliko ya nafsi ya usimulizi (narrative voice) yangeweza pia kujibiwa kwa njia hii; kwa mfano, kuchanganya "narrative voice" ni sifa mojawapo ya tendi-simulizi.

2.6 Swali la "Liyongo aliishi lini" ingefaa litanguliwe na lile la "Je, Liyongo alipata kuishi?" Kama alipata kuishi, tupewe ushahidi.

3.0 **TAMATI**

3.1 Mwandishi amejitosa katika uwanja wa tendi-simulizi bila kujiandaa vizuri. Nahisi kuwa

hajayasoma sana maandishi yaliyo katika uwanja huo, wala hana habari na migogoro mikali iliyomo (k.m. mgogoro kuhusu "African epic", mgogoro wa kina Parry na Lord kuhusu "Oral Style", n.k.). Kwa sababu ya upungufu huu makala yake yanapwaya. Aidha, hajasoma makala ya akina J. Mbele na wengine katika *Jarida la Kiswahili*, *Research in African Literatures*, n.k.) ambayo yangemfunua macho.

3.2 Nia ya maoni haya ni kumsaidia mwandishi ajiendeleze katika uwanja huu aliouchagua. Nia si kumkatisha tamaa. Hivyo, pamoja na uhakiki niliotoa hapo juu, bado nahisi makala haya yana mbegu yenye tunu ambayo inapaswa kurutubishwa ili izae matunda. Hivyo kuna mawili yanayoweza kufanywa:

(a) Makala yasahihishwe lugha na mhariri na kuchapishwa katika *Mulika* bila kubadilishwa sana ili kuendeleza mjadala.

(b) Makala yarejeshwe kwa mwandishi ili ayarekebishe na kuyakamilisha, halafu yachapishwe.

***TANBIHI:***

*Wahariri waliuona umuhimu na uzito wa rai zilizotolewa na msomaji. Hali kadhalika wahariri walikabiliwa na ugumu wa mawasiliano na mwandishi wa makala, yaani Bw. Kithaka wa Mberia. Kwa kuwa, kimsingi, makala ni nzuri na inalijadili suala ambalo lina mguso wa aina yake katika Fasihi ya Kiswahili, wahariri wameamua kuvichapisha vyote viwili: yaani, makala na maoni yake, kwa faida ya mwandishi na wasomaji wengine ambao watapenda kukipigia mbizi kipengele hicho.*

*Wahariri: AMK/JSM*